IJUE RASIMU YA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA YA MWAKA 2014 KWA LUGHA RAHISI



KIMETOLEWA NA
CHAMA CHA SHERIA TANGANYIKA

KIMEANDALIWA NA

Kamati Maalum ya Katiba ya Chama cha Wanasheria Tanganyika ambayo ina wajumbe wafuatao:

Wakili Mpale Mpoki - Mwenyekiti

Wakili James Jesse - Mjumbe

Wakili Issa Maige - Mjumbe

Wakili Godwin Mussa - Mjumbe

Wakili Alex Mgongolwa - Mjumbe

Stephen Msechu - Katibu wa Kamati

HAKIMILIKI 2014 TLS

Si ruhusa kwa kutumia au kutengeneza kwa jinsi au namna yeyote kijarida hiki bila ruhusa ya maandishi kutoka kwa Chama Cha Sheria Tanganyka.

TOLEO LA PILI

WAFADHILI: Ford Foundation

YALIYOMO

UTANGULIZI vii
Katiba ni Nini? vii
Nani Anapaswa Kutunga Katiba? vii
Je, Utungaji wa Katiba Mpya Tanzania Umefanywa na Wananchi? vii
SASA IJUE RASIMU YA KATIBA 1

SURA YA I 1
KUHUSU MUUNDO WA MUUNGANO 1
Mambo ya Muungano 2
Njia za Kulinda Muungano 2

SURA YA 2 4
MISINGI YA KITAIFA, MALENGO YA TAIFA NA MIIKO YA VIONGOZI 4
Tunu za Taifa 4
Ukuzaji wa Maslahi ya Wananchi Na Misingi ya Kidemokrasia 4
Malengo Makuu ya Kitaifa na Mwelekeo wa Sera za Taifa 4
Maadili na Miiko ya Uongozi na Utumishi wa umma 6
Misingi ya Uongozi: 6
Kanuni za Uongozi wa Umma: 7
Miiko ya Uongozi wa Umma 7

SURA YA 3 9
ZIJUE HAKI ZA BINADAMU ZILIZO KATIKA RASIMU 9
Njia ya Kudai Haki za Binadamu 12
Je, Serikali Yaweza kuweka Mipaka katika Haki za Binadamu? 12
Ujue Wajibu Wako Na Wajibu Wa Serikali 12
Wajibu wa Raia 12
Wajibu wa Serikali 13

SURA YA 4 14
JE, NANI NI RAIA WA TANZANIA? 14
Uraia wa kuzaliwa Unapatikanaje? 14

Uraia wa Kuandikishwa Unapatikanaje? 15
Je, inaruhusiwa kuwa na Uraia wa Nchi Mbili (Dual Citizenship)? 15

SURA YA 5 16
VIONGOZI WAKUU WA SERIKALI: Rais, Makamu WA Rais
Na Baraza la Mawaziri 16
Mamlaka na Madaraka ya Rais 16
Sifa za Kuchaguliwa kuwa Rais 16
Je Mtu anaweza kupinga matokeo ya Uchaguzi wa Rais? 17
Makamu wa Rais 17
Baraza la Mawaziri 18
Sifa za Kuteuliwa kuwa Waziri 18
Mwanasheria Mkuu, Katibu Mkuu Kiongozi na Makatibu Wakuu 18

SURA YA 6 19
BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO 19
Idadi ya Wabunge 19
Sifa za Kuchaguliwa kuwa Mbunge 20
Kukosa Sifa za kuwa Mbunge 20
Kupoteza Ubunge 21
Uwezo wa Wapiga kura kumuondoa Mbunge wao 21
Spika na Naibu Spika 21

SURA YA 7 22
MAHAKAMA ZA JAMHURI YA MUUNGANO 22
Majaji wa Mahakama ya Juu na Upatikanaji wao 22
Tume ya Utumishi wa Mahakama 23
Mamlaka ya Mahakama ya Juu 23
Majaji wa Mahakama ya Rufani na Upatikanaji wao 24
Nidhamu na Uwajibikaji wa Majaji 24
Misingi ya Utoaji Haki 24

SURA YA 8 26
VYOMBO VINGINE MUHIMU VILIVYOMO KATIKA RASIMU 26
Tume ya Utumishi wa Umma 26

Majukumu ya Tume 26
Wajumbe wa Tume na Upatikanaji Wao 27
Tume Huru ya Uchaguzi 27
Wajumbe wa Tume 27
Sifa za Kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Tume 27
Kamati ya Uteuzi wa Tume Huru ya Uchaguzi 28
Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi 28
Msajili wa Vyama vya Siasa 29
Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji 29
Tume ya Haki za Binadamu 30

SURA YA 9 32
TAASISI NYINGINEZO 32
Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali 32
Mfuko Mkuu wa Hazina 32
Vyanzo vya Mapato ya Jamhuri ya Muungano 32
Benki Kuu 32
Vyombo vya Ulinzi na Usalama wa Taifa..... 33

SURA YA 10 34
MENGINEYO 34
Watumishi wa Umma Wasioruhusiwa Kuwa Viongozi wa Kisiasa 34
Masharti ya Mpito 43

SHUKRANI

Hiki ni Kijitabu kidogo kilichoandaliwa na Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) kwa ajili ya Elimu ya Uraia kwa Watanzania wote. Kitabu hiki kinaelezea Rasimu ya Pili ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 2014 kwa lugha rahisi ili kutoa fursa kwa wananchi kuelewa mambo muhimu yaliyomo katika Rasimu. Tunatambua kuwa Rasimu ni kubwa sana maana ina Ibara 271 zilizo katika kurasa zaidi ya 100 ambapo sio kila mtu anaweza kupata Rasimu na kuisoma na hata akiwa nayo anaweza kushindwa kuisoma yote na kuielewa kwa urahisi kwa kuwa ni kubwa.

Kwa hiyo basi, madhumuni ya kuandika kitabu hiki ni kusaidia kuongeza uelewa wa mambo yaliyoandikwa katika Rasimu ya Katiba kwa wananchi na hata wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba. Tunategemea watapenda kusoma kitabu hiki. Wananchi wakielewa mambo yaliyomo katika Rasimu wataweza kushiriki vizuri zaidi katika mjadala wa utengenezaji wa Katiba mpya na pia wataweza kushiriki vema katika hatua ya mwisho ya upigaji kura ya maoni.
Chama cha Wanasheria Tanganyika kinafahamu kuwa Bunge Maalum la Katiba laweza kubadili, kurekebisha au kuboresha mambo yaliyotajwa katika Rasimu, lakini tunaamini kuwa kabla ya kupiga kura ya maoni, tunaweza kupata fursa ya kuwaelimisha wananchi tofauti itakayokuwepo kati ya mambo yaliyomo katika Rasimu kwa sasa na mambo yatakayokuwemo baada ya Bunge Maalum kumaliza kazi yake ya kuchambua na hatimaye kupata Katiba Mpya itakayokuwa inapendekezwa kwa ajili ya kupigiwa kura ya maoni.

Kitabu hiki kimeandaliwa na Kamati Maalum ya Katiba ya Chama cha Wanasheria Tanganyika ambayo ina wajumbe wafuatao:

i) Wakili Mpale Mpoki - Mwenyekiti
ii) Wakili James Jesse - Mjumbe
iii) Wakili Issa Miage - Mjumbe
iv) Wakili Godwin Musa - Mjumbe
v) Wakili Alex Mgongolwa - Mjumbe
vi) Stephen Msechu - Katibu wa Kamati

Kamati inapenda kutoa shukrani za dhati kwa uongozi wa TLS chini ya Rais wake Wakili Francis Stolla kwa kutoa *support* kubwa wakati Kamati ilipokuwa ikiendesha vikao na mikutano yake. Chama cha wanasheria pia

kinatoa shukrani za dhati kwa mfadhli wetu mkuu, Ford Foundation, kwa kutuweza kifedha kufanikisha mradi wa Katiba na hata kuandika kitabu hiki. Tunaamini kuwa kijitabu hiki kitasomwa na watu wengi na hatimaye malengo yetu yaweza kufikiwa. Ndugu msomaji, tunakutakia usomaji mzuri!

IJUE RASIMU YA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA YA MWAKA 2014

UTANGULIZI

Katiba ni Nini?

Katiba ndio sheria mama ya nchi. Hii ina maana kwamba Katiba ndio huzaa vyombo vyote vikuu vya Nchi, kuanzia Serikali, Bunge, Mahakama, Vyombo vya Ulinzi na Usalama na hata Tume mbalimbali za Nchi. Katiba pia hutaja Haki za Binadamu na hivyo kutoa ulinzi wa haki za wananchi. Sheria nyingine zote za nchi zinazotungwa sharti zisikiuke Katiba.

Katiba ndio Mwongozo mkuu wa Nchi; kama Katiba itaandaliwa vizuri itaweza kulinda maslahi ya wananchi. Kwa mfano, Katiba ikisema kila mtu ana haki ya kupewa elimu, haki ya matibabu na kuwa na afya bora, na kwamba Serikali itawajibika kwa wananchi, basi ni lazima Serikali iheshimu agizo hilo la katiba.

Nani Anapaswa Kutunga Katiba?

Utungaji wa Katiba ni tofauti na utungaji wa sheria zingine. Katiba hupaswa kutungwa na kuandikwa na wananchi wenyewe. Hii ni kwasababu wananchi ndio msingi wa mamlaka yote. Na Serikali na vyombo vyote vinapata madaraka na mamlaka yao kutoka kwa wananchi ambao kwa umoja wao ndio wamiliki wa Katiba. Ndio maana kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania, utungaji wa Katiba umeshirikisha wananchi moja kwa moja. Kwa hili, tunampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kutoa fursa hii katika utawala wake.

Je, Utungaji wa Katiba Mpya Tanzania Umefanywa na Wananchi?

Swali hili linaweza kujibiwa "NDIYO" au "HAPANA". Ni 'Ndiyo' kwakuwa Rais ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuzingatia sheria, aliteua Tume iliyoongozwa na Mh. Jaji Joseph Warioba mwezi April mwaka 2012 ambayo ilizunguka nchi nzima ili kupata mawazo ya wananchi juu ya kupata Katiba mpya ya

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanayoitaka. Baada ya kupata mawazo hayo, Tume iliandaa Rasimu ya Kwanza. Rasimu hii ilijadiliwa katika Mabaraza ya Katiba ya Wilaya na Mabaraza Maalum na mapendekezo ya kuiboresha yalitolewa. Baada ya hapo Tume ilirutubisha Rasimu ya Kwanza na kutoa Rasimu ya Pili tarehe 30 Desemba 2013 ambayo ilikabidhiwa kwa Mh. Rais.

Kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83, Bunge Maalum la Katiba limekaa kuanzia tarehe 18 Februari 2014 kwa ajili ya kujadili tena Rasimu hiyo na hatimaye kupitisha Rasimu ya mwisho ambayo italetwa kwa wananchi ili wapige kura ya kuikubali au kuikataa (referendum). Kwa kweli utaratibu huu ni mzuri na wa kidemokrasia kwani ni mara ya kwanza kutumika nchini Tanzania.

Hata hivyo kuna mashaka ikiwa matakwa ya wananchi yatazingatiwa. Kama Bunge Maalum la Katiba lisingetokana na wabunge na vyama vya siasa, bali wananchi wasiofungamana na siasa, kungekuwa na uhakika wa kupata Katiba nzuri. Kama mjuavyo kulikuwa na malumbano kabla hata Bunge lenyewe halijaanza, vyama vya siasa vinataka kutumia sera zao kama dira ya kupata Katiba mpya. Kwahiyo hatuna uhakika kama Katiba itakayopatikana baada ya Mkutano huo wa Bunge Maalum itakuwa inaakisi matakwa ya wananchi ama la, ndio maana hatuwezi kusema kama Katiba mpya itakuwa ni mawazo ya wananchi. Kama mabishano makali na kurushiana vijembe vimeanza kutawala Bunge Maalum la Katiba wakati wanatengeneza Kanuni za kuwaongoza, je itakuwaje watakapoanza kujadili Rasimu nzima ya Katiba? Tunaomba busara itumike ili kutatua kutoelewana kwa baadhi ya wajumbe na hatimaye kupata maridhiano yatakayoweka mazingira ya kupata Katiba nzuri.

SASA IJUE RASIMU YA KATIBA

ANGALIZO: IFAHAMIKE KUWA MAELEZO YALIYOKO KATIKA KITABU HIKI YANATOKANA NA RASIMU YA PILI YA KATIBA KAMA ILIVYOPENDEKEZWA NA TUME YA MABADILIKO YA KATIBA. KWA HIYO ISICHULIWE KUWA HIVI NDIVYO KATIBA MPYA YA TANZANIA ITAKAVYOKUWA. MAMBO TULIYOELEZA HAPA YAWEZA KUBADILIKA IKIWA BUNGE MAALUM LA KATIBA LITAPENDEKEZA VINGINEVYO.

SURA YA I

KUHUSU MUUNDO WA MUUNGANO

Tume ya Mabadiliko ya Katiba chini ya Mh. Jaji Joseph Warioba ilipewa hadidu za rejea za kutengeneza Rasimu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika hadidu hizo za rejea Tume ilielekezwa kuwa ihifadhi na kudumisha Muungano na kuhakikisha kuwepo kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwahiyo kulikuwa hakuna uwezekano wa kupendekeza muundo wa serikali moja. Kwakuwa swala la Muungano limekuwa ni jambo tete kabla na hata wakati wa kukusanya maoni, Tume ilipokea maoni mengi kutoka Tanzania Bara na Zanzibar kuhusu aina ya Muungano.

Baadhi ya watu walitoa maoni, wengine walipendekeza kuwe na Nchi moja ya Tanzania yenye Serikali moja ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar isiwepo. Wengine wakapendekeza kuendelea kuwepo kwa mfumo wa Serikali mbili, ambapo kunakuwa na Serikali ya Muungano ambayo inafanya kazi za Tanzania Bara (Tanganyika) na pia inafanya kazi za Muungano na pia kunakuwa na Serikali ya Zanzibar ambayo inafanya kazi za Zanzibar. Kundi la tatu likapendekeza uwepo wa Nchi moja ya Tanzania yenye Serikali tatu. Serikali ya kwanza ni ya Muungano ambayo itafanya kazi za Muungano tu, Serikali ya Pili ni ya Tanzania Bara ambayo itafanya kazi za Tanzania Bara tu (yaani Tanganyika) na Serikali ya tatu ni ya Zanzibar kama ilivyo sasa. Kundi la nne ambalo wengi wao ni wananchi kutoka Zanzibar wakapendekeza Muungano uwe wa nkataba (mkataba). Hii ikiwa na maana kuwa Tanganyika na Zanzibar kila moja ijitegemee kama nchi huru, ila tushirikiane katika mambo fulani fulani kwa muda maalum.

Tume ya Jaji Warioba baada ya kutafakari mapendekezo yote hayo na kuzingatia matatizo au kero mbalimbali ambazo zimedumu kwa muda mrefu, ambapo kila sehemu ya Muungano inashutumu upande mwingine kuwa unafaidika zaidi, ikapendekeza katika Rasimu kuwa na muundo wa SHIRIKISHO, ambapo tutaendelea kuwa na NCHI MOJA yenye Serikali tatu; Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Tanganyika (Ib. 60). [Ib. ni kifupi cha neno "Ibara"]

Mambo ya Muungano

Ibara ya kwanza ya Rasimu ya Katiba inaeleza kuwa Hati ya Makubaliano ya Muungano ndio msingi mkuu wa Muungano wetu. Na kwa mujibu wa Rasimu hiyo Serikali ya Muungano itakuwa na jukumu la kutekeleza mambo saba tu ya Muungano. Mambo mengine yote yatakuwa chini ya Nchi Washirika (yaani Tanganyika na Zanzibar). Na mambo hayo yametajwa katika ukurusa wa mwisho wa Rasimu. Mambo hayo ni:

- Katiba na Mamlaka [za Kikatiba] ya Jamhuri ya Muungano,
- Ulinzi na Usalama,
- Uraia na Uhamiaji,
- Sarafu na Benki Kuu,
- Mambo ya Nje,
- Usajili wa Vyama vya Siasa, na
- Ushuru wa Bidhaa na Mapato yasiyo ya kodi yatokanayo na Mambo ya Muungano [maduhuli].

Njia za Kulinda Muungano

Ili kulinda na kudumisha Muungano wetu, kuna vipengele ambayo vimewekwa katika Rasimu, navyo ni kama ifuatavyo:

i) Ukuu wa Katiba: Katiba ya Muungano itakuwa ndio sheria kuu. Katiba za nchi Washirika sharti zizingatie masharti ya Katiba hii (Ib. 8)

ii) Kila Nchi Mshirika itazingatia misingi ya ushirikiano na kuzingatia haki na usawa kwa ajili ya ustawi ulio bora wa wananchi (Ib. 65)

iii) Utendaji wa Serikali wa Nchi Washirika utatekelezwa kwa kuzingatia umoja wa Jamhuri ya Muungano, nia, umuhimu na azma ya kukuza umoja wa kitaifa na kudumisha heshima ya Taifa na Muungano (Ib. 66)

iv) Kila Nchi Mshirika itateua Waziri Mkazi atakayeratibu na kusimamia mahusiano baina ya Serikali za Nchi Washirika na pia Serikali ya Muungano (Ib. 67)

v) Kila kiongozi mkuu katika mamlaka ya utendaji atakuwa na wajibu wa kulinda, kuimarisha na kudumisha Muungano. Na viongozi wafuatao kabla ya kushika madaraka yao wataapa kutetea na kudumisha Muungano. Hao ni Rais wa Muungano, Makamu wake, Rais wa Tanganyika na Rais wa Zanzibar (Ib. 69)

vi) Kutakuwa na Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali ambayo wajumbe wake ni Makamau wa Rais, Rais wa Tanganyika, Rais wa Zanzibar, Mawaziri Wakaazi na Waziri wa Mambo ya Nje ambao jukumu lao kubwa ni kukuza na kudumisha Muungano na kutatua migogoro itakayojitokeza (Ib. 109, 110)

vii) Mahakama ya Juu (Supreme Court) itakuwa na uwezo wa kusikiliza na kuamua migogoro itokanayo na Muungano (Ib. 156).

SURA YA 2

MISINGI YA KITAIFA, MALENGO YA TAIFA NA MIIKO YA VIONGOZI

Tunu za Taifa

Rasimu ya Katiba inatamka Tunu zifuatazo ambazo sharti zienziwe na kuzingatiwa:

- Utu
- Uzalendo
- Uadilifu
- Umoja
- Uwazi
- Uwajibikaji, na
- Lugha ya Taifa (ambayo ni Kiswahili) (Ib. 5).

Ukuzaji wa Maslahi ya Wananchi Na Misingi ya Kidemokrasia

Rasimu inaweka misingi ifuatayo:

- Wananchi ndio msingi wa mamlaka yote,
- Lengo kuu la Serikali ni kuleta maendeleo na ustawi wa wananchi,
- Serikali itawajibika kwa wananchi,
- Ushirikishwaji wa wananchi (Ib. 6),
- Utu, heshima na haki za binadamu sharti zithaminiwe, kulindwa na kudumishwa,
- Sheria za nchi zisimamiwe na kutekelezwa,
- Ardhi ambayo ni rasilimali kuu sharti ilindwe, itunzwe na kutumiwa na wananchi wa Tanzania kwa manufaa, maslahi na ustawi wao na vizazi vyao vijavyo,
- Kuwepo kwa fursa na haki sawa kwa wananchi wote bila ubaguzi kati ya mwanaume na mwanamke au sababu nyingine za kibaguzi,
- Aina zote za dhuluma, vitisho, unyanyasaji, rushwa, uoenevu, ubaguzi au upendeleo unakomeshwa,
- Nchi iongozwe kwa kufuata misingi ya demokrasia, utawala bora na utawala wa sheria (Ib. 7).

Malengo Makuu ya Kitaifa na Mwelekeo wa Sera za Taifa

Ibara ya 10 ya Rasimu inaweka malengo makuu la Kitaifa na hatua ambazo hazina budi kuchukuliwa na Serikali ili kutimiza malengo hayo. Malengo Makuu kwa mujibu wa Katiba ni "Kulinda, kuimarisha na kudumisha HAKI, UDUGU, AMANI, na UMOJA kwa kuzingatia USTAWI wa wananchi na kujenga Taifa huru lenye DEMOKRASIA, UTAWALA BORA, MAENDELEO ENDELEVU na KUJITEGEMEA.

Ili kutimiza Malengo hayo kuna hatua za kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kimazingira ambazo hazina budi kuchukuliwa na Serikali.

Serikali itawajibika kutoa taarifa Bungeni kila mwaka kuhusu utekelezaji wa hatua hizo (Ib. 11). Hatua hizo ni nyingi sana. Hapa tutataja chache tu:

(a) Hatua za Kisiasa

- Kuhakikisha uwepo wa amani, kujenga utamaduni wa ushirikiano na uvumilivu wa kisiasa,
- Kuzuia, kupinga na kuondoa dhuluma, vitisho, ubaguzi, rushwa, upendeleo na uonevu,
- Kuhakikisha ustawi, ulinzi na usalama wa watu na mali zao.

(b) Hatua za Kijamii

- Kuhakikisha heshima na haki za binadamu zinadumishwa kwa misingi ya Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu,
- Kuhakikisha kuwa vyombo vyote vya Serikali vinatoa fursa sawa kwa kila raia bila kujali itikadi, jinsi, au sababu nyingine za kibaguzi,
- Kuhakikisha kuwa msaada na hifadhi ya jamii inatolewa kwa wasiojiweza, wazee, wagonjwa, watoto na watu wenye ulemavu,
- Kuwezesha upatikanaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa wasiomudu gharama za uwakili.

(c) Hatua za Kiuchumi

- Kuwaletea wananchi maisha bora kwa kuondoa umaskini,
- Kuhakikisha shughuli za Serikali zinatekelezwa kwa manufaa ya wananchi wote na kuzuia unyonyaji,

- Kuweka mazingira bora ya kufanya biashara na kutoa fursa za uwekezaji,
- Kuweka mazingira bora ya kukuza kilimo, ufugaji na uvuvi na utafutaji wa masoko,
- Kusimamia mizania ya bei ya mazao na pembejeo.

(d) Hatua za Kiutamaduni

- Kulinda na kuhifadhi urithi wa asili, malikale na sehemu za kihistoria,
- Kulinda, kuhifadhi na kuendeleza tamaduni za jamii mbalimbali ambazo hakizinzani na sheria na sera za nchi,
- Kulinda na kuendeleza lugha ya Kiswahili.

(e) Hatua za kimazingira

- Kuhakikisha kuwa ni wajibu wa kila mtu kulinda na kudumisha mazingira kwa faida yetu na kizazi kijacho,
- Kuhakikisha kuwa taasisi za umma na asasi za kiraia zinawajibika kusimamia, kuhifadhi na kulinda mazingira kwa mujibu wa sheria,
- Kuhakikisha kuwa wananchi ndio wenye haki ya kumiliki rasilimali za kijenetiki za Tanzania kwa manufaa ya Taifa.

Maadili na Miiko ya Uongozi na Utumishi wa umma

Kwa kuzingatia kuwa kumekuwa na tatizo la kuporomoka kwa maadili kwa baadhi ya viongozi na watumishi wa umma na kutumia madaraka na mamlaka zao kujinufaisha, Rasimu imeweka misingi ya uongozi na utumishi, kanuni za uongozi na miiko ya uongozi.

Misingi ya Uongozi:

- ❖ Madaraka au Uongozi ni dhamana na sharti madaraka hayo yatumike kwa kuzingatia Katiba, kuheshimu wananchi, kukuza hadhi ya Taifa na kulinda heshima ya ofisi na kukuza imani na heshima kwa wananchi.
- ❖ Uteuzi katika nafasi za madaraka uzingatie misingi ya uwezo, sifa, na mwenendo wa mtu na kwa nafasi za uchaguzi, uchaguzi uwe huru na wa haki.
- ❖ Kusiwepo upendeleo katika kufanya uamuzi kwa misingi ya ukabila, udini, upendeleo, rushwa, ubaguzi au udugu.
- ❖ Utoaji wa huduma usiwe na upendeleo, bali ufuate misingi ya uwazi, ukweli, uaminifu na kutangaza maslahi binafsi pale ambapo kuna mgongano wa kimaslahi.
- ❖ Uwajibikaji kwa umma.
- ❖ Uadilifu, nidhamu na kujituma katika kazi (Ib. 13).

Kanuni za Uongozi wa Umma:

- ❖ Kiongozi wa umma, wakati wote atahakikisha kuwa mwenendo wake—
  - hauruhusu kutokea kwa mgongano wa maslahi yake binafsi na maslahi ya umma,
  - hauhatarishi maslahi ya umma,
  - haushushi hadhi ya ofsi anayofanyia kazi (Ib. 14)
- ❖ Endapo kiongozi wa umma atapewa zawadi akiwa anatekeleza wajibu wake, atalazimika kuwasilisha zawadi hiyo kwa Katibu Mkuu Kiongozi kupitia kwa Katibu Mkuu wa Wizara au kiongozi wa taasisi anayotoka (Ib. 15),
- ❖ Kiongozi wa umma hatafungua au kumiliki akaunti ya benki nje ya Tanzania isipokuwa tu kwa masharti yatakayowekwa na sheria (Ib. 16),
- ❖ Kiongozi wa umma hataomba wala kupokea mkopo au faida yoyote ambayo inashusha hadhi au heshima ya utumishi wa umma (Ib. 16),
- ❖ Kila kiongozi wa umma (kwa mujibu wa sheria) atalazimika kutangaza na kuwasilisha kwa Tume ya Maaadili ya Uongozi na Uwajibikaji, ndani ya siku 30 baada ya kupata uongozi na siku 30 baada ya kuacha uongozi, mali zake na thamani zake, za mwenza wake na watoto wake wa chini ya mika 18 na madeni kama yapo (Ib. 17),
- ❖ Kiongozi wa umma hatashiriki katika kufanya uamuzi wa jambo ambalo ana maslahi nalo, au lina maslahi kwa mwenza wake, mtoto wake, jamaa yake, rafiki yake, au mtu mwingine wa karibu,
- ❖ Itakuwa ni marufuku kwa kiongozi wa umma kushiriki katika uamuzi unaohusu kuongeza au kuboresha maslahi yanayohusu wadhifa alionao. Endapo atashiriki, basi maslahi hayo hayatamhusu yeye bali yatamhusu kiongozi atakayekuja baada yake,
- ❖ Kiongozi wa umma hataruhusiwa kushika nafasi za madaraka zaidi ya moja au kutumikia mihimili ya dola zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja (Ib. 18),
- ❖ Kiongozi wa umma hataruhusiwa kutumia au kuruhusu kutumika kwa mali ya umma kwa manufaa yake binafsi (Ib. 19).

Miiko ya Uongozi wa Umma

Miiko ya Uongozi wa Umma imetajwa katika Sehemu ya Pili ya Sura ya Pili kuanzia Ibara ya 21. Rasimu inatamka kuwa, kiongozi wa umma atapaswa kuheshimu na kutii maadili ya viongozi (kama ilivyo katika Sheria) pamoja na miiko ya uongozi. Kiongozi wa umma atabanwa na miiko ifuatayo: Ya kwamba—

- ❖ Hatopaswa kuvunja au kukiuka masharti ya Katiba.
- ❖ Hatopaswa kutoa au kupokea rushwa.
- ❖ Hatopaswa kujilimbikizia mali kinyume cha sheria.

- ❖ Hatopaswa kusema uongo au kutoa taarifa sizizo za ukweli.
- ❖ Hatatakiwa kutoa siri za Serikali kinyume cha sheria.
- ❖ Hatakiwi kutumia wadhifa, nafasi au cheo chake kwa manufaa binafsi au manufaa ya familia yake, ndugu, jamaa, rafiki au mtu yeyote aliye na uhusiano naye wa karibu.
- ❖ Hatopaswa kufanya vitendo vya uzembe, uvivu, ubaguzi, kiburi, dharau au unyanyasaji wa kijinsia.
- ❖ Atapaswa kuheshimu na kuendeleza dhana ya uwajibikaji wa pamoja ikiwa anahusika na dhana hiyo (kwa mfano, mawaziri).
- ❖ Atapaswa kuwa na tabia na mienendo inayokubalika katika jamii.
- ❖ Atapaswa kuheshimu, kutunza na kulinda mali za umma.
- ❖ Atapaswa kutenganisha biashara na shughuli binafsi na masuala yanayohusiana na uongozi. (Ib. 21).

Rasimu pia inaweka masharti yafuatayo katika utumishi na uongozi wa umma. Kwamba,

- ❖ Ikiwa kiongozi wa umma atatuhumiwa kwa makosa ya kimaadili, wizi, udhalilishaji wa mtu mwingine au wa kijinsia, au ubadhirifu wa mali ya umma basi atasimamishwa kazi hadi suala lake litakapoamuliwa kwa mujibu wa sheria au taratibu zilizowekwa.
- ❖ Mtumishi wa umma aliye katika ajira ya kudumu hataruhusiwa kuingia katika ajira nyingine yoyote ya kudumu yenye malipo ya mshahara.
- ❖ Mtumishi wa umma hataruhusiwa kugombea, kuchaguliwa au kuteuliwa kushika nafasi ya madaraka katika chama cha siasa au kushika nafasi ya madaraka ya kisiasa.
- ❖ Hata hivyo, endapo mtumishi wa umma ataamua kugombea, kuchaguliwa au kuteuliwa katika nafasi hizo za kisiasa, basi utumishi wake utakoma (Ib. 22).

SURA YA 3

ZIJUE HAKI ZA BINADAMU ZILIZO KATIKA RASIMU

Rasimu imezingatia Haki zote za Binadamu zilizoko katika Katiba ya Mwaka 1977 na kuongeza haki nyingine nyingi.

Haki zifuatazo zimetajwa katika Rasimu kuanzia Ibara ya 23 hadi ya 48:

i) Usawa wa Binadamu. Kwamba, binadamu wote ni sawa (Ib. 23).

ii) Haki ya Kuishi. Kwamba, kila mtu anayo haki ya kuishi kwa mujibu wa sheria (Ib. 24).

iii) Uhuru dhidi ya Ubaguzi. Kwamba, watu wote ni sawa mbele ya sheria na wana haki sawa bila ya kubaguliwa.

iv) Haki ya Kukata rufaa au kupata nafuu nyingine ya kisheria.

v) Haki ya kutoadhibiwa kwa kitendo ambacho wakati kinatendeka hakikuwa kosa, au kupewa adhabu ambayo sio kwa mujibu wa sheria.

vi) Haki ya kutoteswa, kufanyiwa ukatili au kupewa adhabu za kutweza au kudhalilisha (Ib. 25).

vii) Haki ya kutokuwa mtumwa, au kusafirishwa katika biashara ya kuuza binadamu (Ib. 26).

viii) Haki ya kuishi kama mtu huru na kutokamatwa na kuwekwa kizuizini isipokuwa kwa mujibu wa sheria (Ib. 27).

ix) Haki ya faragha, kutoingiliwa katika mawasiliano yako binafsi, na kupata usalama wa nafsi yako, mali yako, maskani yako na familia yako (Ib. 28).

x) Uhuru wa mtu kwenda anakotaka katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au nje ya nchi na kurudi, isipokuwa tu pale uhuru huo utakapozuiliwa kwa mujibu wa sheria (Ib. 29).

xi) Uhuru wa maoni. Kwamba, kila mtu ana haki ya kuwa na maoni, kufanya mawasiliano, kueleza fikra zake, kupewa taarifa na kufanya ugunduzi, ubunifu na utafiti (Ib. 30).

xii) Uhuru wa kila mtu kutafuta, kupata, kutumia na kusambaza habari au taarifa, na uhuru wa kuanzisha vyombo vya habari (Ib. 31).

xiii) Uhuru wa Imani ya dini. Kwamba, kila mtu anao uhuru wa imani, kuchagua na kubadilisha imani ya dini, kutangza dini, kufanya ibada na kueneza dini (Ib. 32).

xiv) Uhuru wa mtu kujumuika na kushirikiana na watu wengine. Hii ni pamoja na uhuru wa kutoa mawazo hadharani, kuanzisha na kujiunga na vyama vya siasa au mashirika/taasisi sizizo za kiserikali (Ib. 33).

xv) Haki ya kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi ama moja kwa moja au kupitia wawakilishi (Ib. 34).

xvi) Haki ya kufanya kazi. Kwamba, kila mtu na haki ya kuajiriwa au kujiajiri katika kazi yoyote halali (Ib. 35).

xvii) Haki za wafanyakazi: Ambazo ni pamoja na haki ya kupata ujira na malipo yanayoendana na kazi kwa usawa, kuunda, kujiunga na kushiriki katika chama cha wafanyakazi, kupitia chama kufanya majadiliano na kuingia mikataba na mwajiri ya hali bora ya kazi (Ib. 36).

xviii) Haki ya kumiliki mali na hifadhi ya mali yako kwa mujibu wa sheria, isipokuwa kwa mali ambayo haikupatikana kihalali (Ib. 37).

xix) Haki ya uraia. Kila mtu kutambuliwa uraia wake. Na haki ya wananchi kupata cheti cha kuzaliwa, kitambulisho cha uraia na passport (endapo inahitajika) (Ib. 38).

xx) Haki za mtu aliyewekwa kuzuizini; kama vile kuelezwa sababu za kukamatwa, kuwasiliana na wakili au ndugu, kutolazimishwa kutoa maelezo, kupelekwa mahakamani mapema, mfungwa kupata nakala ya hukumu (Ib. 39).

xxi) Haki ya mtu aliyekamatwa na kuwekwa chini ya ulinzi, kupewa haki zote za binadamu. Ikiwa Raia anapelekwa nje ya nchi kujibu

mashtaka au kuhojiwa sharti taratibu za kisheria zifuatwe kama vile extradition (Ib. 40).

xxii) Haki ya kuishi katika mazingira safi na salama (Ib. 41).

xxiii) Haki ya kupata Elimu bora. Kwa Elimu ya msingi sharti iwe bure na iliyo kamilifu. Kwa shule binafsi, sharti gharama ziwe nafuu (Ib. 42).

xxiv) Haki ya Mtoto. Ambazo ni pamoja na kupewa jina na uraia, kutoa mawazo na kusikilizwa, kucheza na kupata elimu, kupata lishe bora na huduma za afya, kupata malezi na ulinzi bila ya ubaguzi (Ib. 43).

xxv) Haki na wajibu wa Vijana. Haki ya kushiriki katika shughuli za maendeleo na kuwekewa mazingira wezeshi kushiriki katika shughuli za kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni (Ib. 44).

xxvi) Haki za watu wenye Ulemavu. Ambazo ni pamoja na kuheshimiwa, kupata elimu kwa kutumia vifaa maalum, kushiriki shughuli za kijamii, kuwekewa miundombinu wezeshi, kutumia lugha za alama, maandishi ya nukta nundu au yaliyokuzwa, kupata ajira n.k (Ib. 45).

xxvii) Haki za makundi madogo katika Jamii ambazo ni jamii za watu wanaoishi kiasili. Haki hizo ni haki ya kushiriki katika uongozi, kupewa fursa maalum za elimu, kiuchumi na ajira, kutengewa maeneo yao ya ardhi ambayo kwa desturi makundi hayo hutumia na kuishi (Ib. 46).

xxviii) Haki za wanawake. Ambazo ni pamoja na kuheshimiwa utu wao, kuwa salama dhidi ya vitendo vya kinyonyaji, udhalilishaji na ukatili, kushiriki katika uchaguzi na ngazi zote za maamuzi, kupata fursa ya ajira sawa na wanaume, kupata huduma bora ya afya n.k (Ib. 47).

xxix) Haki za Wazee. Ambazo ni kupata fursa ya kushiriki katika shughuli za kijamii, kuendeleza maisha yao, kutambuliwa utu wao na kuheshimiwa, na kupata mahitaji ya msingi kutoka familia zao, jamii na Serikali (Ib. 48).

xxx) Haki ya kufaidi haki zote za msingi za binadamu, haki ya kupata hifadhi sawa chini ya sheria (Ib. 52).

Zingatio: Ibara ya 53 (3) inasema kuwa Mikataba yote ya kikanda na kimataifa ya haki za binadamu ambayo Tanzania imeridhia itakuwa sehemu ya Haki za Binadamu katika Katiba yetu. Mfano wa mikataba hiyo ni kama vile Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa mwaka 1966, Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kijamii, Kiuchumi na Kiutamaduni wa mwaka 1966, Mikataba ya Kimataifa ya Haki za Watoto, Wanawake na Watu wenye ulemavu, Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Haki za Watu wa mwaka 1981 n.k.

Njia ya Kudai Haki za Binadamu

Ibara ya 54 inasema kuwa mtu yeyote anayeamini kuwa haki yake imekiukwa au inataka kukiukwa na mamlaka, chombo cha uamuzi, sheria au sera, anaweza kufungua shauri katika Mahakama Kuu kwa hati maalum. Na mahakama ikiona yafaa inaweza kutoa zuio, katazo, maelekezo inayoona yanafaa au kuamuru jambo fulani lifanyike ili kutoa nafuu inayohitajika. Kesi za aina hii zaweza kufunguliwa na mtu anayejiwakilisha mwenyewe au taasisi inayowakilisha watu, au kusaidiwa na mwakilishi au mtu ambaye anawakilisha kundi la watu wenye malengo yanayofanana.

Je, Serikali Yaweza kuweka Mipaka katika Haki za Binadamu?
Ikiwa Serikali inataka kuweka mipaka katika Haki za Binadamu, Rasimu inatamka kuwa sharti mipaka hiyo itumike kwa **uwazi** na kwa kuzingatia **demokrasia, utu, usawa, uhuru** na **vigezo vingine** ambavyo ni:

- Aina ya haki husika,
- Umuhimu na sababu za kuweka mipaka,
- Asili (nature) na ukubwa wa mpaka husika,
- Uhusiano baina ya mpaka husika na sababu ya kuweka mpaka,
- Njia nyepesi zaidi ya kufikia madhumuni ya kuweka mpaka husika, na
- Umuhimu wa kulinda usalama wa nchi (Ib. 55).

Ujue Wajibu Wako Na Wajibu Wa Serikali

Wajibu wa Raia
Mara nyingi haki hufuatana na wajibu. Rasimu imeweka wajibu wa Raia kuwa, kila raia ana wajibu wa:

- Kulinda na kutetea Katiba na sheria za nchi,
- Kulinda na kuheshimu Tunu za Taifa,
- Kulipa kodi,
- Kuheshimu haki, uhuru na maslahi ya watu wengine,
- Kuilinda nchi yetu na kushiriki katika ulinzi wa Taifa,
- Kulinda na kuheshimu utamaduni na maadili ya Taifa,
- Kulinda na kutunza mazingira (Ib. 49),
- Kushiriki kwa kujituma na kwa umanifu katika kazi halali,
- Kuwa na nidhamu ya kazi na kujitahidi kufikia malengo ya uzalishaji mali ya binafsi na malengo ya pamoja (Ib. 50),
- Kulinda maliasili ya taifa, mali ya mamlaka ya nchi, mali ya jamii na kuheshimu mali ya mtu mwingine,

- ❖ Kulinda, kuhifadhi na kudumisha rasilimali za nchi na maliasili ya Taifa, na
- ❖ Kutunza vizuri mali ya umma na mali inayomilikiwa kwa pamoja na kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhirifu (Ib. 51).

Wajibu wa Serikali

Kwakuwa watekelezaji wakubwa wa haki za binadamu ni Serikali, basi Rasimu imeweka wajibu kwa mamla zote za nchi kama ifuatavyo:

- ❖ Wajibu wa Serikali na mamlaka zote kuzingatia, kuheshimu, kuhifadhi na kudumisha haki za binadamu.
- ❖ Wajibu wa kuheshimu na kuzingatia mikataba ya kikanda na kimataifa ya haki za binadamu ambayo Tanzania imeridhia, isipokuwa tu yale masharti ambayo Tanzania imeeleza wazi kutojifunga nayo (Ib. 53).

SURA YA 4

JE, NANI NI RAIA WA TANZANIA?

Rasimu inasema kuwa, mtu yeyote ambaye ni Raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atendelea kuwa raia chini ya Katiba mpya. Rasimu inatamka kuwa uraia wa Tanzania ni wa aina mbili; au unapatikana kwa njia mbili, nazo ni: kwa **kuzaliwa** au **kujiandikisha** (Ib. 56).



Uraia wa kuzaliwa Unapatikanaje?

i) Mtu yeyote anayezaliwa Tanzania (yaani Tanganyika au Zanzibar) atakuwa raia wa kuzaliwa endapo, wakati wa kuzaliwa, mama au baba yake ni au alikuwa Raia wa Tanzania.

ii) Mtu anayezaliwa nje ya Tanzania atakuwa raia wa kuzaliwa ikiwa mama au baba yake ni raia wa Tanzania.

iii) Endapo mzazi wa mtoto alifariki kabla ya mtoto kuzaliwa, kama mzazi huyo alikuwa ni Mtanzania, basi mtoto atakuwa Mtanzania.

iv) Mtoto yeyote chini ya miaka saba akikutwa ndani ya Tanzania na wazazi wake hawajulikani, basi mtoto huyo atakuwa raia wa Tanzania , vinginevyo ibainike kuwa wazazi wake sio raia (Ib. 57).

Uraia wa Kuandikishwa Unapatikanaje?

i) Mtu ambaye si raia lakini amekuwa mkaazi wa Tanzania na kutimiza masharti yote ya kisheria anaweza kuomba kuandikishwa kuwa raia.

ii) Mtu aliyefunga ndoa na raia wa Tanzania anaweza kuomba kuandikishwa kuwa raia endapo amedumu katika ndoa hiyo kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo na pia amekuwa mkaazi na kutimiza masharti yote ya kisheria.

iii) Kama mtoto wa chini ya miaka 18, ambaye sio raia wa Tanzania, akiasiliwa na raia wa Tanzania basi atapata uraia wa kuandikishwa (ib. 58)

Je, inaruhusiwa kuwa na Uraia wa Nchi Mbili (Dual Citizenship)?

Rasimu ya Katiba haijatambua uraia wa nchi mbili. Hata hivyo, Ibara ya 59 imetoa hadhi maalum kwa watu ambao wana asili au nasaba ya Tanzania. Inasema kuwa, mtu yeyote mwenye asili au nasaba ya Tanzania na ambaye ameacha kuwa raia wa Tanzania baada ya kupata uraia wa nchi nyingine, atakapokuwa Tanzania atakuwa na hadhi maalum kadri itakavyoelezwa na sheria.

SURA YA 5

VIONGOZI WAKUU WA SERIKALI: Rais, Makamu WA Rais Na Baraza la Mawaziri

Mhimili wa kwanza wa Nchi ni Serikali ambayo itaundwa na Rais, Makamu wa Rais na Mawaziri. Madaraka yote ya Serikali yako chini ya Rais, ila yanaweza kukasimiwa kwa Makamu wa Rais au watu wengine katika utumishi wa Serikali (Ib. 70).

Mamlaka na Madaraka ya Rais
Rais wa Jamhuri ya Muungano anabeba kofia tatu: Ndiye Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Mhimili wa Serikali na ni Amiri Jeshi Mkuu (Ib. 71).

Madaraka na majukumu yake katika kofia zote hizo tatu yametamkwa katika Ibara ya 72. Katika utekelezaji wa majukumu yake Rasimu inaweka wajibu kwa Rais kufuata na kuzingatia ushauri atakaopewa na mamlaka za nchi. Na endapo hakubaliani na ushauri aliopewa, sharti atoe sababu katika Baraza la Mawaziri. Rasimu inaeleza kuwa, Rais hatalazimika kufuata ushauri ambao unakwenda kinyume au kukiuka Katiba au sheria za nchi (Ib. 74).

Sifa za Kuchaguliwa kuwa Rais
Ili mtu aweze kugombea na kuchaguliwa kuwa Rais, sharti awe na sifa zifuatazo (Ib. 79):

- Awe raia wa kuzaliwa wa Tanzania.
- Awe na akili timamu.
- Wazazi wake wote wawili wawe ni raia wa kuzaliwa wa Tanzania.
- Awe na umri usiopungua miaka arobaini (40).
- Awe na shahada ya chuo cha elimu ya juu kinachotambuliwa.
- Awe ni mwanachama wa chama cha siasa aliyependekezwa na chama chake au mgombea huru/binafsi.
- Sera zake au sera za chama chake zisiwe za mrengo wa kuligawa Taifa.
- Awe mwadilifu, anayeheshimu haki za binadamu, asiyedharau wala kubagua watu na anafuata maadili ya viongozi na mwenendo wake hautiliwi shaka na jamii.

Ifahamike pia kuwa mtu ataruhusiwa kushika madaraka ya urais kwa vipindi viwili tu vya miaka mitano mitano. Hata hivyo mtu ambaye alikuwa Rais wa Zanzibar au Rais wa Tanganyika anaruhusiwa kugombea kiti cha urais wa Muungano (Ib. 83).

Je Mtu anaweza kupinga matokeo ya Uchaguzi wa Rais?

Sio kila mtu anaruhusiwa kupinga matokeo ya uchaguzi wa urais baada ya kutangazwa na Tume ya Uchaguzi. Bali mtu aliyegombea nafasi hiyo katika uchaguzi mkuu na hakuridhika na matokeo anaweza kuwasilisha malalamiko yake katika Mahakama ya Juu (Supreme Court). Endapo Mahakama ya Juu itaamua kuwa matokeo ya Uchaguzi wa Rais si halali, uchaguzi wa Rais utarudiwa ndani ya siku sitini (60) baada ya uamuzi huo (Ib. 81).

Makamu wa Rais

Makamu wa Rais ndiye Msaidizi Mkuu wa Rais. Atapatikana kwa utaratibu kama unaotumika sasa hivi ambapo anakuwa ni mgombea mwenza wa mgombea urais. Sifa za kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais ni zile zile za Rais. Endapo itatokea, kwa sababu yoyote ile, kiti cha Urais kiko wazi basi Makamu wa Rais atashika madaraka ya Urais.

Baraza la Mawaziri

Kwa kuzingatia muundo wa Shirikisho wenye Serikali tatu, na kwakuwa Serikali ya Muungano inashughulikia mambo saba tu, basi Rasimu imeweka idadi maalum ya Mawaziri na Naibu Mawaziri. Jumla yao wote haitazidi kumi na tano (15). Rais wa Jamhuri ya Muungano akishauriana na Makamu wa Rais atateua Mawaziri ambao kabla ya kuapishwa ni lazima wathibitishwe na Bunge. Katika uteuzi Rais atazingatia uwakilishi wa Nchi Washirika (Ib. 98).

Chini ya Rasimu hii, kutakuwa na nafasi ya Waziri atakayeitwa Waziri Mwandamizi. Huyu atateuliwa na Rais na kuthibitishwa na Bunge (Ib. 99). Na atafanya kazi kama vile Waziri Mkuu, kwani ndiye atakuwa na madaraka ya uthibiti na usimamizi wa utekelezaji wa shughuli za Serikali za kila siku na atatekeleza majukumu yake kadri atakavyoelekezwa na Rais (Ib. 100).

Sifa za Kuteuliwa kuwa Waziri

Rasimu inaweka utenganisho wa madaraka kati ya Serikali na Bunge. Kwahiyo basi mtu akiwa mbunge hatakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Waziri au Naibu Waziri. Ili mtu ateuliwe kuwa Waziri anapaswa kuwa na sifa hizi:

- ❖ Awe ni raia wa kuzaliwa wa Tanzania.
- ❖ Awe na shahada ya chuo cha elimu ya juu kinachotambulika.
- ❖ Awe na uweledi na uzoefu.

Mwanasheria Mkuu, Katibu Mkuu Kiongozi na Makatibu Wakuu

Rais amepewa mamlaka ya kuteua Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu Kiongozi na Makatibu Wakuu wa Wizara.

Rais aweza kumteua mtu yeyote mwenye sifa za uwakili wa mahakama kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutoka miongoni mwa watumishi waandamizi katika utumishi wa umma na baada ya hapo lazima athibitishwe na Bunge (Ib. 104).

Katibu Mkuu Kiongozi atapatikana miongoni mwa watumishi waandamizi wa umma ambapo Tume ya Utumishi wa Umma itapendekeza kwa Rais majina ya watu watatu naye ateteua mmojawapo na baadaye kuthibitishwa na Bunge (Ib. 105).

Tume ya Utumishi wa Umma pia itapendekeza kwa Rais watu wanaofaa kuteuliwa kuwa Makatibu Wakuu au Naibu Makatibu Wakuu kutoka miongoni mwa watumishi waandamizi katika utumishi wa umma. Hawa hawahitaji kuthibitishwa na Bunge (Ib. 106).

SURA YA 6

BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO

Idadi ya Wabunge

Mhimili wa pili wa Nchi ni Bunge. Rasimu inapendekeza njia tofauti na ilivyo sasa katika kupata Bunge la Jamhuri ya Muungano. Kama ilivyo kwa mawaziri, idadi ya wabunge wa Bunge la Muungano imepunguzwa kwakuwa kutakuwa na Bunge la Tanganyika ambalo litapatikana kwa mujibu wa Katiba ya Tanganyika endapo muundo wa Serikali tatu utakubalika. Jumla ya wabunge wote wa Bunge la Muungano ni wabunge sabini na tano (75) tu ambapo watakuwa kama ifuatavyo:

- Kutakuwa na wabunge sabini (70) wa kuchaguliwa kutoka majimbo ya Uchaguzi yatakayowekwa na Tume ya Uchaguzi. Kati yao, wabunge hamsini (50) watatoka Tanzania Bara (Tanganyika) na ishirini (20) watatoka Zanzibar.
- Kila jimbo la uchaguzi litakuwa na nafasi mbili za ubunge. Moja ya kwa ajili ya mwanamke na ya pili kwa ajili ya mwanaume. Kwa maana hiyo, Tanganyika itakuwa na majimbo ishirini na tano (25)

na Zanzibar majimbo kumi (10). Wabunge wote watapigiwa kura na wananchi na kwahiyo viti maalum vya wanawake havitakuwepo.

- Wabunge watano (5) wengine watapatikana kutoka kundi la watu wenye ulemavu ambao watateuliwa na Rais (Ib. 113).

Sifa za Kuchaguliwa kuwa Mbunge

Mtu atakuwa mbunge kwa vipindi vitatu tu vya miaka mitano mitano. Mtu yeyote atakuwa na sifa za kugombea ubunge au kuteuliwa kuwa mbunge kama ni mlemavu ikiwa ana sifa zifuatazo:

- Awe ni raia wa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka ishirini na moja (21).
- Awe anajua kusoma na kuandika lugha ya Kiswahili au Kiingereza na pia ana elimu isiyopungua kidato cha nne.
- Awe ama ni mwanachama wa chama cha siasa au mgombea huru/ binafsi.
- Awe ni mtu mwadilifu na anayeheshimu haki za binadamu na asiyedharau wala kubagua watu (Ib. 125).

Kama ilivyo kwa nafasi ya Rais, Rasimu imeweka ukomo wa ubunge kuwa ni vipindi vitatu tu.

Kukosa Sifa za kuwa Mbunge

Rasimu inasema kuwa mtu atapoteza sifa za kuwa mbunge kutokana na mojawapo ya sababu zifuatazo:

- Mtu huyo aliwahi kuwa mbunge kwa vipindi vitatu vya miaka mitano.
- Imethibitika kuwa mtu huyo ana ugonjwa wa akili.
- Mtu huyo amehukumiwa na Mahakama yoyoye na kupewa adhabu ya kifo au kufungwa gerezani kwa muda unaozidi miezi sita kwa kosa lolote.
- Katika kipindi cha miaka mitano kabla ya kugombea amewahi kuhukumiwa na kupewa adhabu ya kifungo kwa kosa la kukosa uaminifu au kuvunja sheria ya maadili ya uongozi.
- Mtu huyo ana maslahi yoyote katika mkataba wa Serikali aliyowekewa miiko na endapo amekiuka miiko hiyo.
- Mtu huyo anashika madaraka ya ofisa mwandamizi katika utumishi wa umma.
- Mtu aliyezuiwa kujiandikisha kuwa mpiga kura au kupiga kura kwa mujibu wa sheria.
- Amewahi kutiwa hatiani mahakamani kwa kosa la kukwepa kodi katika kipindi cha miaka mitano kabla ya uchaguzi (Ib. 125).

Kupoteza Ubunge

Wabunge wamewekewa masharti ambayo endapo mbunge atakiuka atapoteza sifa ya kuwa mbunge. Mbunge atakoma kuwa mbunge ikiwa:

- ❖ Atapoteza sifa ya kuwa mbunge kutokana na sababu zilizotajwa hapo juu.
- ❖ Atakosa kuhudhuria Mikutano ya Bunge miwili mfululizo bila ruhusa ya Spika.
- ❖ Itathibitika kuwa amevunja Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.
- ❖ Atashindwa kufanya kazi za mbunge kwa muda wa miezi sita mfululizo kutokana na maradhi au kuwekwa gerezani.
- ❖ Atashindwa kutoa tamko rasmi kuhusu mali zake kwa mujibu wa Katiba na sheria.
- ❖ Atajiuzulu ubunge.
- ❖ Ataamua kwa ridhaa yake kujiondoa katika chama chake cha siasa, au akifukuzwa au kuvuliwa uanachama na chama chake.
- ❖ Atafariki dunia (Ib. 128).

Uwezo wa Wapiga kura kumuondoa Mbunge wao

Sambamba na hayo hapo juu, wapiga kura nao wamepewa mamlaka ya kumuondoa mbunge wao madarakani kwa mujibu wa masharti yatakayowekwa baadae na sheria, ikiwa mbunge atafanya lolote kati ya haya yafutayo:

- ❖ Endapo ataunga mkono sera ambazo zinaenda kinyume na maslahi ya wapiga kura wake au maslahi ya Taifa.
- ❖ Endapo atashindwa kuwasilisha au kutetea kwa dhati hoja zinazotokana na kero za wapiga kura wake.
- ❖ Endapo ataacha kuishi au kuaamua kuhamisha makazi yake kutoka jimbo lake la uchaguzi kwa zaidi ya miezi sita bila sababu za msingi, au
- ❖ Litokeapo jambo jingine litalowekwa na sheria (Ib. 129)

Spika na Naibu Spika

Mtu atachaguliwa kuwa Spika au Naibu Spika endapo ana angalau elimu ya chuo kikuu na awe na umri usiopungua miaka arobaini (40). Ili kuleta usawa, kupunguza upendeleo na kuondoa manung'uniko miongoni mwa wabunge, Rasimu inapendekeza kuwa mtu atakayegombea kiti cha Spika au Naibu Spika asiwe mbunge na wala asiwe kiongozi au kuwahi kuwa kiongozi wa juu wa chama cha siasa katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya kuomba kuchaguliwa (Ib. 132, 133, 134 na 135). Spika na Naibu Spika watachaguliwa kwa msingi kuwa endapo Spika atatoka Tanganyika basi Naibu Spika atatoka Zanzibar au kinyume chake.

SURA YA 7

MAHAKAMA ZA JAMHURI YA MUUNGANO

Mahakama ni mhimili wa tatu ambao ni muhimu sana katika upatikanaji wa haki. Rasimu imependekeza mabadiliko katika muundo wa Mahakama. Kwa kuzingatia pendekezo la kuwa na Serikali tatu, Nchi Washirika ndio zitakuwa na Mahakama Kuu na zile mahakama zilizo chini yake. Serikali ya Jamhuri ya Muungano itakuwa na mahakama mbili za juu ambazo ni:

- Mahakama ya Juu (Supreme Court) na chini yake kutakuwa na
- Mahakama ya Rufani (Court of Appeal) (Ib. 153).



Majaji wa Mahakama ya Juu na Upatikanaji wao

Mahakama ya Juu itakuwa na Majaji wafuatao ambao watapatikana kwa kuzingatia uwakilishi wa Zanzibar na Tanganyika:

- Jaji Mkuu ambaye atakuwa ndiye Rais wa Mahakama ya Juu na pia ndiye Mkuu wa Mhimili wa Mahakama,
- Naibu Jaji Mkuu ambaye atakuwa Makamu wa Rais wa Mahakama hii, na

- ❖ Majaji wengine wasiopungua saba (Ib. 154).

Jaji Mkuu atateuliwa na Rais kutoka orodha ya majina ya watu watatu (3) watakaopendekezwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama na atathibitishwa na Bunge (Ib. 158). Naibu Jaji Mkuu atateuliwa kwa utaratibu huo huo (Ib. 159).

Majaji wengine wa Mahakama ya Juu watateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa majina yatakayopendekezwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama lakini hawatahitaji kuthibitishwa na Bunge (Ib. 160). Jaji wa Mahakama ya Juu atastaafu akifikisha umri wa miaka sabini (70).

Tume ya Utumishi wa Mahakama inaelekezwa kuwa katika mchakato wa uteuzi wa majina ya watu kuteuliwa kuwa majaji sharti izingatie uwazi (Ib. 181). Rasimu haiko wazi kama watu wanaotaka ujaji watatakiwa kuomba kazi na kuhojiwa.

Tume ya Utumishi wa Mahakama

Tume ya Utumishi wa Mahakama itakuwa na wajumbe wafuatao ambao watateuliwa na Rais:

- ❖ Jaji Mkuu ambaye atakuwa Mwenyekiti,
- ❖ Jaji mmoja wa Mahakama ya Juu,
- ❖ Jaji mmoja wa Mahakama ya Rufani,
- ❖ Mwakilishi wa Chama cha Wanasheria Tanganyika,
- ❖ Mwakilishi wa Chama cha Wanasheria Zanzibar,
- ❖ Wawakilishi wawili wa vitivo vya sheria kutoka vyuo vikuu, mmoja kutoka Tanganyika na mwingine kutoka Zanzibar watakaopendekezwa na vyuo vyao,
- ❖ Mtendaji Mkuu wa Mahakama, ambaye atakuwa Katibu (Ib. 180).

Mamlaka ya Mahakama ya Juu

Watakapokuwa wakilisiliza shauri watakaa majaji watano na watakuwa na mamlaka ya rufani. Rasimu haielezi kama kuna wakati watakapokuwa wanatoa maamuzi watalazimika kukaa majaji wengi zaidi, aidha saba au tisa. Hili linaweza kuwekwa na Kanuni za mahakama. Ila Rasimu inaeleza kuwa watakuwa na mamlaka ya awali na ya mwisho katika kuamua matokeo ya uchaguzi wa Rais na pia ikiwa wataombwa kufanya hivyo watakuwa na uwezo wa kutoa ushauri kwa Serikali au Serikali za Nchi Washirika kuhusu swala lolote la kisheria (Ib. 156).

Majaji wa Mahakama ya Rufani na Upatikanaji wao
Mahakama ya Rufani itakuwa na majaji wafuatao kwa kuzingatia uwakilishi wa pande zote za Muungano:

- ❖ Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani,
- ❖ Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani, na
- ❖ Majaji wengine wasiopungua kumi na saba (Ib. 165).

Uteuzi wa Majaji wote wa Mahakama ya Rufani utafanywa na Rais kwa kufuata utaratibu ule ule wa majaji wa Mahakama ya Juu, isipokuwa tu Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Mahakama hii hawatathibitishwa na Bunge (Ib. 169, 170, 171). Na jaji wa mahakama hii pia atastaafu afikishapo umri wa miaka sabini.

Nidhamu na Uwajibikaji wa Majaji
Majaji wote wamewekewa ulinzi dhidi ya kuondolewa katika nafasi zao. Rasimu imeweka utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya majaji ya Mahakama ya Juu na Mahakama ya Rufani. Jaji ya Mahakama ya Juu au Rufani anaweza kuondolewa katika nafasi ya madaraka ya ujaji na Rais kwa sababu za kushindwa kutekeleza madaraka yake kutokana na:

- ❖ Maradhi,
- ❖ Tabia mbaya inayoathiri maadili ya kazi ya jaji au sheria inayohusu maadili ya viongozi wa umma,
- ❖ Kukiuka kanuni za maadili ya majaji (Ib. 164 na 175).

Hata hivyo, ili kumuondoa jaji madarakani kutokana na sababu hizo hapo juu utaratibu ufuatao utafuatwa:

i) Rais anaweza, baada ya kushauriana na Jaji Mkuu kumsimamisha kazi jaji huyo,

ii) Rais atateua Tume ya Majaji yenye wajumbe wasiopungua watatu kutoka nchi yoyote ya Jumuiya ya Madola ambao watachunguza shauri hilo,

iii) Baada ya kufanya uchunguzi Tume hiyo itamshauri Rais kama jaji huyo anayehusika aondolewe madarakani ama la, na

iv) Endapo Tume itamshauri Rais kuwa jaji aliyechunguzwa aondolewe au asiondolewe madarakani basi Rais anapaswa kufuata ushauri huo.

Misingi ya Utoaji Haki
Rasimu inatamka kuwa Mahakama ndiyo chombo chenye mamlaka ya mwisho ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Ib. 150)

na katika kutoa uamuzi katika kesi za madai au jinai zitazingatia kanuni zifuatazo:

- ❖ Kutenda haki kwa wote bila kujali hali ya mtu kijamii, kisiasa, kiutamaduni au kiuchumi.
- ❖ Kutochelewsha haki bila sababu za msingi.
- ❖ Kutoa fidia ipasavyo kwa watu walioathirika kutokana na makosa ya watu wengine.
- ❖ Kukuza na kuendeleza usuluhishi baina ya wanaohusika katika migogoro, na
- ❖ Kutenda haki bila kufungwa na masharti ya kiufundi (Ib. 151).

SURA YA 8

VYOMBO VINGINE MUHIMU VILIVYOMO KATIKA RASIMU

Tume ya Utumishi wa Umma
Rasimu inapendekeza kuwe na Tume ya Utumishi wa Umma ambayo ni chombo muhimu sana katika utumishi wa umma.

Majukumu ya Tume
Pamoja na majukumu mengine, Tume itakuwa na majukumu makuu yafuatayo:

- ❖ Kumshauri Rais juu ya uteuzi wa viongozi katika nafasi mbalimbali kwa mujibu wa Katiba,
- ❖ Kuteua watu kuhudumu au kushikilia kwa muda utumishi katika ofisi za umma,
- ❖ Kuunda na kupanga ngazi za mishahara na marupurupu ya watumishi wa umma, ikiwemo viongozi wa kisiasa, watumishi katika Utumishi wa Serikali, Bunge na Mahakama, na

- ❖ Kudurusu na kusawazisha mishahara na marupurupu ya watumishi wa umma ikiwemo viongozi wa kisiasa, watumishi katika Utumishi wa Serikali, Bunge na Mahakama (Ib. 188)

Wajumbe wa Tume na Upatikanaji Wao

Tume ya Utumishi wa umma itakuwa na Wajumbe wafuatao ambao watateuliwa na Rais na kuidhinishwa na Bunge:

- ❖ Mwenyekiti, na
- ❖ Wajumbe Wengine Sita.

Sifa za mtu kuteuliwa kuwa Mwenyekiti au Mjumbe wa Tume ni kuwa:

- ❖ Awe ni raia wa Tanzania,
- ❖ Awe na shahada ya chuo kikuu,
- ❖ Awe na uzoefu wa utumishi wa umma, upeo mkubwa katika mambo ya utumishi, utawala na mambo ya jamii kwa kipindi kisichopungua miaka kumi (10), na
- ❖ Awe na heshima, uweledi, uaminifu, uadilifu na asiye na tabia au mwenendo wenye kutiliwa shaka na jamii (Ib. 186).

Tume Huru ya Uchaguzi

Wajumbe wa Tume

Rasimu inapendekeza kuundwa kwa tume inayoitwa "Tume Huru ya Uchaguzi" ambayo wajumbe wake watateuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na **Kamati ya Uteuzi** na hatimaye kuthibitishwa na Bunge. Tume itakuwa na wajumbe wafuatao:

- ❖ Mwenyekiti,
- ❖ Makamu Mwenyekiti, na
- ❖ Wajumbe wengine saba (Ib. 190)

Sifa za Kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Tume

Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi sharti kuwa na sifa zifuatazo:

- ❖ Awe ni raia wa kuzaliwa wa Tanzania,
- ❖ Awe ni mtu aliyewahi kushika nafasi ya Ujaji na ameshika nafasi hiyo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano (5),
- ❖ Awe ni mwaminifu, mwadilifu na mwenye mwenendo usiotiliwa shaka na jamii,
- ❖ Awe ni mtu ambaye hajawhi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai linalohusiana na uaminifu (Ib. 190).

Mjumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi awe na sifa zifuatazo:

- ❖ Awe ni raia wa kuzaliwa wa Tanzania,

- ❖ Awe ni mtu mwaminifu, mwadilifu, na mwenye mwenendo usiotiliwa shaka na jamii,
- ❖ Awe ni mtu ambaye hajawahi kushika nafasi ya madaraka yoyote katika chama cha siasa,
- ❖ Awe na shahada ya chuo kikuu kinachotambulika,
- ❖ Awe ni mtu ambaye hajawhi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai lilalohusu kukosa uaminifu (Ib. 190).

Watu Wasio na Sifa za Kuteuliwa kuwa Wajumbe ni:
- ❖ Mbunge, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi au Diwani, au
- ❖ Mtu ambaye ni mtumishi wa umma.

Kamati ya Uteuzi wa Tume Huru ya Uchaguzi
Kama tulivyosema hapo juu, wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi watapatikana kutoka miongoni mwa majina yatakayopendekezwa kwa Mh. Rais na Kamati ya Uteuzi. Kamati ya Uteuzi itakuwa na jukumu la kupokea na kuchambua majina ya watu walioomba kazi au waliopendekezwa kuwa wajumbe na mtu yeyote ikiwemo asasi zisizo za kiserikali. Kamati ya uteuzi itakuwa na wajumbe wafuatao:

- ❖ Jaji Mkuu ambaye atakuwa ni Mwenyekiti,
- ❖ Spika wa Bunge ambaye atakuwa Makamu Mwenyekiti,
- ❖ Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar,
- ❖ Spika wa Bunge la Tanganyika,
- ❖ Jaji Mkuu wa Zanzibar,
- ❖ Jaji Mkuu wa Tanganyika, na
- ❖ Mwenyekiti wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji (Ib. 191).

Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi
Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi ambaye ndiye mtendaji mkuu wa kila siku wa shughuli za Tume atashughulikia masuala ya uchaguzi, uandikishaji wa wapiga kura na uendeshaji wa kura ya maoni (Ib. 196). Mkurugenzi atateuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Tume ya Utumishi wa Umma na hatimaye kuthibitishwa na Bunge (Ib. 195).

Ili mtu ateuliwe kuwa Mkurugenzi wa Tume Huru ya Uchaguzi atapaswa kuwa na sifa zifuatazo:
- ❖ Awe ni raia wa kuzaliwa na angalau mzazi wake mmoja awe ni raia wa kuzaliwa wa Tanzania,
- ❖ Awe ni mtu mwaminifu, mwadilifu, na mwenye mwenendo

usiotiliwa shaka na jamii,
- ❖ Awe ni mtu ambaye hajawahi kushika nafasi ya madaraka yoyote katika chama cha siasa,
- ❖ Awe na shahada ya chuo cha elimu ya juu,
- ❖ Awe ni mtu ambaye hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai linalohusu kukosa uaminifu.

Msajili wa Vyama vya Siasa

Msajili wa Vyama vya Siasa atateuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Tume ya Utumishi wa Umma na baadaye kuthibitishwa na Bunge (Ib. 198). Ili mtu ateuliwe kuwa Msajili wa Vyama vya Siasa anapaswa kuwa na sifa kama zile za kuteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi tulizotaja hapo juu.

Kazi na wajibu wa Msajili wa Vyama vya Siasa ni kama ifuatavyo:
- ❖ Kusimamia na kuratibu uandikishaji na shughuli za vyama vy siasa,
- ❖ Kutayarisha na kuchapisha taarifa za kila mwaka kuhusu ripoti za ukaguzi wa fedha kwa kila chama cha siasa,
- ❖ Kusimamia fedha za vyama vya siasa (Ib. 199).

Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji

Ili kusimamia vizuri maadili ya viongozi, Rasimu inapendekeza kuanzishwa kwa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji (Ib. 200). Tume hii itakuwa na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wengine wasiozidi saba watakaoteuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Kamati Maalum ya Uteuzi (Ib. 200). Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti lazima wathibitishwe na Bunge.

Kamati Maalum ya Uteuzi kwa ajili ya kupata wajumbe wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji itakuwa na wajumbe wafuatao:
- ❖ Jaji Mkuu wa Tanzania,
- ❖ Spika wa Bunge la Muungano,
- ❖ Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanganyika,
- ❖ Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar,
- ❖ Spika wa Bunge la Tanganyika,
- ❖ Spika wa Baraza la Wawikilishi Zanzibar, na
- ❖ Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Ib. 202).

Sifa za kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Tume hii ni kama ifuatavyo:
- ❖ Awe ni raia wa kuzaliwa wa Tanzania,
- ❖ Awe ni mtu mwenye shahada ya chuo cha elimu ya juu,
- ❖ Awe ni mtu mwenye uzoefu katika utumishi wa umma kwa kipindi kisichopungua miaka 15 kwa mwenyekiti na makamu wake au miaka

10 kwa mjumbe wa kawaida,

- ❖ Awe ni mtu mwenye heshima, weledi, uaminifu,uadilifu na asiye na tabia na mwenendo wenye kutiliwa shaka na jamii, na
- ❖ Awe ni mtu ambaye hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai linalohusu kukosa uaminifu (Ib. 200 na 201).

Baadhi ya kazi za Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji ni hizi zifuatazo:

i) Kufuatilia na kuchunguza tabia na mwenendo wa viongozi na watumishi wa umma,

ii) Kusimamia Maadili na Miiko ya Uongozi wa umma na watumishi wa umma,

iii) Kusimamia sheria za nchi kuhusu maadili na uwajibikaji wa viongozi wa umma na watumishi wa umma,

iv) Kutoa ushauri juu ya masuala ya ubadhirifu wa fedha kwa mamlaka husika,

v) Kufanya upekuzi kwa kiongozi wa umma anayepewa dhamana kabla ya kuingia madarakani (majukumu yako mengi, tazama Ibara ya 203).

Tume ya Haki za Binadamu

Kama ilivyo katika Katiba ya sasa ya Mwaka 1977, kutakuwa na Tume ya Haki za Binadamu ambayo itakuwa na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wasiozidi saba ambao watateuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Kamati Maalum ya Uteuzi (Ib. 208). Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti watashika madaraka baada ya kuthibitishwa na Bunge.

Kamati ya Uteuzi kwa ajili ya kuteua wajumbe wa Tume ya Haki za Binadamu itakuwa na wajumbe wafuatao:

- ❖ Jaji Mkuu wa Tanzania,
- ❖ Spika wa Bunge la Muungano,
- ❖ Spika wa Bunge la Tanganyika,
- ❖ Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar,
- ❖ Jaji Mkuu wa Tanganyika,
- ❖ Jaji Mkuu Zanzibar, na
- ❖ Mwenyekiti wa Tume ya Maadili na Uwajibikaji (Ib. 209)

Ili mtu ateuliwe kuwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Mjumbe wa Tume sharti awe na sifa zifuatazo:

i) Awe ni raia wa kuzaliwa (ikiwa ni Mwenyekiti au Makamu

Mwenyekiti). Kwa mjumbe awe ni raia tu (ama wa kuzaliwa au kujiandikisha),

ii) Kwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti lazima wawe na shahada ya sheria kutoka chuo cha elimu ya juu. Kwa mjumbe sharti awe na shahada ya chuo cha elimu ya juu bila kujali ni ya sheria,

iii) Awe ni mtu mwenye kuheshimu haki za binadamu,

iv) Kwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti awe mtu mwenye uzoefu wa utumishi wa umma, upeo mkubwa katika mambo ya haki za binadamu, utawala na mambo ya jamii kwa kipindi kisichopungua miaka kumi,

v) Awe mtu mwenye heshima, weledi, uaminifu, uadilifu na asiye na tabia au mwenendo wenye kutiliwa shaka na jamii (Ib. 208).

Majukumu ya Tume ya Haki za Binadamu yameorodheshwa katika Ibara ya 210.

SURA YA 9

TAASISI NYINGINEZO

Zaidi ya ofisi au taasisi tulizokwisha tajwa hapo juu, Rasimu pia inapendekeza kuanzishwa kwa taasisi na vyombo vifuatayo:

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
Huyu atateuliwa na Rais na kuthibitishwa na Bunge (Ib. 215). Hata hivyo, Rais atamteua kutoka katika orodha ya majina matatu ya watumishi wa umma yatakayopendekezwa na Tume ya Utumishi wa Umma (Ib. 216). Kazi na majukumu yake yametajwa katika Ibara ya 217.

Mfuko Mkuu wa Hazina
Kutakuwa na Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali ambao fedha zote zinazopatikana zitawekwa (Ib. 221). Ibara ya 222 inaweka masharti ya namna ya kutoa fedha hizo na matumizi yake.
Kuhusu ***Deni la Taifa na Mikopo ya Serikali***, Rasimu inaweka masharti yafuatayo:

- Kwamba Deni la Taifa litadhaminiwa na Mfuko Mkuu wa Hazina.
- Kwamba Bunge linaweza kutunga sheria ambayo:
  - i) Itaweka masharti ya kuzingatiwa na Serikali wakati wa kukopa,
  - ii) Itaweka ukomo wa deni la Taifa na madhumuni ya deni hilo, na
  - iii) Itaweka utaratibu wa Serikali kutoa taarifa Bungeni kuhusu mikopo ya Serikali na Deni la Taifa litokanalo na mikopo hiyo (Ib. 227-228).

Vyanzo vya Mapato ya Jamhuri ya Muungano vimetajwa katika Ibara ya 231. Vyanzo hivyo ni:

i) Ushuru wa bidhaa,
ii) Mapato yasiyo ya kodi yanayotokana na taasisi za Muungano,
iii) Mchango kutoka Nchi Washirika,
iv) Mikopo kutoka ndani na nje ya Nchi,
v) Mapato mengineyo.

Benki Kuu
Benki Kuu itakuwa na majukumu ya kutoa sarafu, kudhibiti na kusimamia mzunguko wa sarafu, kuandaa na kusimamia sera na mipango ya sarafu, kusimamia na kudhibiti fedha za kigeni na kusimamia Benki za Nchi Washirika (Ib. 233).

Nchi Washirika (Tanganyika na Zanzibar) zinaruhusiwa kuwa na Benki zao (yaani Benki Kuu ndogo) ambazo zitatunza akaunti ya fedha za Serikali hizi, na pia kusimamia sera za kifedha na benki za biashara katika mamlaka zao (Ib. 234).

Vyombo vya Ulinzi na Usalama wa Taifa

Kutakuwa na vyombo vya ulinzi na usalama wa Taifa ambavyo vitafanya kazi katika Jamhuri nzima ya Muungano, navyo ni:

i) Jeshi la Wananchi wa Tanzania,
ii) Jeshi la Polisi,
iii) Idara ya Usalama wa Taifa (Ib. 236)

Mtu yeyote hataruhusiwa kuanzisha taasisi, kampuni, jumuia au shirika linalohusiana na ulinzi na usalama wa Taifa au ushirika wa kijeshi isipokuwa kwa mujibu wa sheria na Katiba. Na endapo Rais anataka kuunda chombo chochote kingine cha ulinzi na usalama sharti ashauriane na Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa.

SURA YA 10

MENGINEYO

Katika Sura ya 16 Rasimu ya Katiba imeweka mambo mengineyo. Hapa tutaja mambo machache tu. Kwanza ni Ibara ya 254 ambayo inatoa tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika Rasimu. Kwa mfano neno Serikali linatafsiriwa kuwa ni "Serikali ya Jamhuri ya Muungano na mtu yeyote anayetekeleza madaraka au mamlaka yoyote kwa niaba ya Serikali". Pili, Rasimu inasema Katiba itakapopitishwa itazinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano na kuanza kutumika (Ib.255).

Watumishi wa Umma Wasioruhusiwa Kuwa Viongozi wa Kisiasa

Jambo jingine muhimu katika sura hii ni kuwa kuna baadhi ya watumishi wa umma ambao pindi wanapoacha kazi au kustaafu hawataruhusiwa kugombea, kuchaguliwa au kuteuliwa katika nafasi za kisiasa hadi muda wa miaka mitatu upite. Watumishi hao ni:

i) Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu, na Jaji yeyote wa Mahakama ya Juu,
ii) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Jaji yeyote wa Mahakama ya Rufani,
iii) Mwanasheria Mkuu wa Serikali,
iv) Spika na Naibu Spika wa Bunge,
v) Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama,
vi) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,
vii) Katibu Mkuu Kiongozi na Makatibu Wakuu wa Wizara,
viii) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, na Wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mkurugenzi wa Uchaguzi,
ix) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu,
x) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji,
xi) Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Umma, na
xii) Msajili wa Vyama vya Siasa (Ib. 253).

Masharti ya Mpito

Sura ya 17 ambayo ndiyo ya mwisho katika Rasimu inaweka masharti ya kipindi cha mpito. Muda au kipindi cha Mpito ni kuanzia siku Katiba Mpya itakapoanza kutumika hadi Disemba 31, mwaka 2018. Baadhi ya mambo ambayo yanatajwa katika Sura hii ni haya yafuatayo:

❖ Sheria zote zilizotungwa na Bunge la sasa la Muungano zinazotumika Bara na Zanzibar na zinazohusu mambo ya Muungano zitaendelea kutumika.

- ❖ Sheria zote zilizotungwa na Bunge la sasa la Muungano zinazohusu Tanzania Bara zitaendelea kutumika Tanganyika.
- ❖ Mtu yeyote anayeshika nafasi ya madaraka itakapoanza kutumika Katiba mpya ataendelea kushika nafasi hiyo kana kwamba anashika madaraka hayo kwa mujibu wa Katiba mpya kwa masharti yaliyowekwa na Ib.260-263.
- ❖ Kutungwa kwa Katiba ya Tanganyika.
- ❖ Kurekebisha Katiba ya Zanzibar ili isipingane na Katiba mpya.
- ❖ Kuweka utaratibu na kufanya mgawanyo wa rasilimali baina ya Serikali ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika.
- ❖ Kuundwa kwa Taasisi zote za Kikatiba kwa mujibu wa Katiba mpya, nk (Ib.269).

Mwisho kabisa Rasimu inapendekeza kuwa na Kamati ya Utekelezaji wa Katiba mpya ambayo itateuliwa na Rais na itakuwa na Mwenyekiti na Wajumbe wengine wanane. Nia ya kuwa na Kamati hii ni kusimamia utekelezaji wa masuala yanayohitaji kufanyiwa kazi na kukamlishwa katika muda wa mpito.

_____TANGANYIKA LAW SOCIETY_____

FORD FOUNDATION

Tanganyika Law Society
Plot No 391, Chato Street, Regent Estate
P.o Box 2148 Dar es Salaam | Tel: +255 22 2775313 | +255 22 550 002
Fax: +255 22 2775314 | Email: info@tls.or.tz | Website: www.tls.or.tz